

UFAFANUZI KUHUSU TARATIBU ZA KUPANDISHWA VYEO KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1.0 Utangulizi

Ndugu msomaji, Ijumaa ya wiki iliyopita tulipata fursa ya kuangalia juhudi za Tume ya Utumishi wa Umma katika kuendeleza watumishi wake kielimu ili kujenga msingi imara wa utekelezaji wa majukumu yake na utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika makala hiyo tulielezwa kuwa, Tume katika kipindi cha mwaka 2005/2006, iliwapeleka watumishi 193 katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Watumishi waliopolekwa katika mafunzo ya muda mrefu walikuwa 133 wakati watumishi waliopolekwa mafunzo ya muda mfupi walikuwa 60. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, 2005/2006 na 2006/2007 Tume iliendesha pia mafunzo kwa Wadau wake 1,885. Katika makala ya leo tutaangalia suala la upandishwaji vyeo Serikalini, jambo ambalo lilijitokeza sana katika wiki ya Utumishi wa Umma iliyoanza tarehe 17/6/2007 – 23/07/2007 ambapo baadhi ya watumishi walilalamika kutopandishwa vyeo katika utumishi wao. Katika makala hii tutaangalia maana ya upandishwaji vyeo na kujadili taratibu za kupandishwa vyeo katika Utumishi wa Umma kabla na baada ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kuanza kutumika katika utumishi wa umma ili kutoa elimu kwa baadhi ya wadau hasa watumishi ambao

bado wana uelewa wa upandishwaji vyeo unaozingatia muda na uzoefu kazini na kuongeza uelewa wa Sheria inayotumika kwa sasa katika masuala ya ajira na nidhamu katika utumishi wa umma.

2.0 Taratibu za kupandishwa vyeo katika Utumishi wa Umma.

Kabla ya kuelezea taratibu zinazopaswa kufuatwa katika kutekeleza jukumu la kupandisha vyeo watumishi wa umma, kwanza napenda kuelezea maana ya upandishwaji vyeo katika utumishi wa umma. Upandishwaji vyeo katika Utumishi wa Umma, kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, ni kupanda daraja kutoka ngazi moja kwenda ngazi ya juu kikazi. Upandishwaji vyeo katika Utumishi wa Umma umepitia hatua mbali mbali; ukiangalia suala la upandishwaji vyeo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8, 2002 utaona kuwa watumishi wa Umma walikuwa wanapandishwa vyeo kwa kuzingatia muda na uzoefu kazini, upandishwaji vyeo ulifanyika kwa msereko. Baada ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8, upandishwaji vyeo unazingatia mambo yafuatayo:

2.1 Sifa na utendaji bora wa kazi

Kulingana na Sheria Na. 8 ya mwaka 2002, mtumishi wa umma hawezi kupanda cheo kwa msereko bali atapanda

cheo kwa kuzingatia sifa, ujuzi, uadilifu na utendaji bora wa kazi. Hivi ndivyo vigezo vinavyoweza kumsaidia mtumishi kupanda cheo. Hii ni changamoto kwa watumishi wa umma; wanapaswa kujiendeleza katika utumishi wao na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuhakikisha kuwa kila kazi wanazozifanya lazima ziwe na matokeo na hivyo kujiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kuangaliwa kupandishwa vyeo.

2.2 Nafasi wazi ya kazi

Hakuna upandishwaji vyeo unaoweza kufanyika bila ya kuwa na nafasi wazi ya kazi. Hivyo mamlaka za ajira/waajiri wanapaswa kutekeleza jukumu hili baada ya kuainisha nafasi iliyo wazi na kuomba kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuruhusu kujaza nafasi iliyo wazi. Aidha katika kubainisha nafasi wazi, inatakiwa pia kuainisha miundo ya utumishi ambayo itakuwa na nafasi zilizo wazi

2.3 Kutenga fedha ya kulipa mishahara

Pamoja na ubainishaji wa nafasi wazi za kazi, mamlaka za ajira zinapaswa pia kutenga fedha katika bajeti ya mwaka ambazo zitamwezesha mwajiri kulipa mishahara ya nafasi wazi za kazi zitakazojazwa.

3.0 Hitimisho

Ndugu msomaji, tunapaswa kuliangalia na kulielewa suala la upandishwaji vyeo lilivyokuwa kabla na lilivyo sasa baada ya

Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kuanza kutumika. Kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hiyo, upandishwaji vyeo ulizingatia Sheria nyingine ambayo iliweka utaratibu wa kupandisha vyeo kwa kuzingatia muda na uzoefu wa kazi au kupanda vyeo kwa **mserereko**. Baada ya kuanza kutumika kwa Sheria Na. 8, 2002, upandishwaji vyeo utazingatia sifa, ujuzi na utendaji bora wa kazi. Aidha, katika kutekeleza suala la upandishwaji vyeo, mamlaka za ajira/Wajiri wanapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu, miongozo na Nyaraka mbali mbali zinazotolewa na serikali.

Ikiwa una maoni, ushauri au maswali tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM

Au piga simu Na. 022 – 2126811 - 4